

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI KIFARU
S.L.P. 163
MWANGA.

TAREHE : 16/12/2020

MAWASILIANO

MKUU WA SHULE: 0755379021
MAKAMU : 0766480744
MATRON : 0672437925
PATRON : 0717411041

KUMB.NA. KHS/ F. KUJI/ VOL.III/2020 /01

Jina la Mwanafunzi

S.L.P.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIFARU WILAYA YA MWANGA
MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021.

1.0. Utangulizi

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika shule hii mwaka **2021** Shule ya Sekondari Kifaru ipo umbali wa km. 1.5mji wa kifaru .

Usafiri wa Pikipiki kutoka mjini Kifaru unapatikana katika kituo cha mabasi cha Kifaru , Nauli ni Tsh. 1,000/=

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **.11/01/2021 na** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021.**

NB: Kutakuwa na kikao cha wazazi wote tarehe **23/01/2021.** saa 3:00 asubuhi

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1 Sare za Shule

Wavulana .

- a) Suruali mbili (2) rangi ya blue zenye mikunjo mawili mbele na upana chini usipungue inchi 17
- b) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
- c) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi .
- d) Sweta 1 rangi ya suruali
- e) Soksi nyeusi jozi mbili

Wasichana

- a) Sketi mbili (2) rangi ya **blue** (Sketi mshono rinda box inchi 7 kutoka gotini/suruali chini inci 16)
- b) Soksi jozi mbili nyeupe (stocking)
- c) Shati mbili nyeupe mikono mifupi/ nusu kanzu kwa waislam
- d) Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba visigino vifupi
- e) Sweta 1 rangi ya sketi
- f) Rangi ya ushungi ifanane na sare za shule (Nusu kanzu) kwa Waislamu imeruhusiwa

Vifaa vya Taaluma.

- 2.3 - Daftari 12 kumbwa, mkebe (mathematical Instruments set)
- Kalamu ya bluu au nyeusi, pencil na rula aje navyo. (wasichana na wavulana)

Vifaa vya Michezo.

Wavulana

- Raba jozi moja (Nyeusi)
- Bukta ya michezo rangi ya bluu na fulana ya bluu isiyo na maandishi wala michoro yeyote

Wasichana.

- Raba jozi moja (Nyeusi)
- Tracksuit bluu na fulana ya bluu isiyo na maandishi na maandishi wala michoro yeyote.

3.0 .Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995 . Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi , yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Raisi –TAMISHEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Nguo za nyumbani haziruhusiwi

3.1. Makosa yafuatayo yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule .

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo .
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.
6. Kusuka nywele kwa wanafunzi hawaruhusiwi
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevywa
9. Uvutaji wa sigara
10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoza au kuolewa.
11. Kupata ujuzito/ kutoa mimba .
12. Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
13. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana .
14. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
15. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
16. Kudharau bendera ya Taifa .
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua , au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
18. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

3.3 . Sheria za Madarasa

1. Mwanafunzi lazima kuhudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa , kwani kutega kipindi inahesabika kuwa ni kosa la utoro ambalo linaweza kumwondoa mwanafunzi shuleni.
2. Kelele za aina yoyote darasani au bwenini zinakatazwa, kwani darasani / bwenini si mahali pa kupiga kelele.
3. Hakuna mwanafunzi yoyote anayeruhusiwa kuandika ubaoni bila ruhusa.
4. Wakati wowote mwalimu akiingia darasani ni lazima wanafunzi wote wasimame kwa heshima na kumwamkia. Halafu mwalimu atatoa ruhusa ya kukaa.
5. Wanafunzi watahakikisha usafi na unadhifu wa darasa lao kila siku kabla ya masomo kuanza.
6. Mwanafunzi lazima afanye mazoezi ya mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake, ni kosa linaloweza kumfukuzisha mwanafunzi shuleni kwa kuacha kufanya mazoezi / mitihani bila sababu za msingi.

Viambatanisho na fomu muhimu .

- i) Fomu ya mapokezi na utambulisho
- ii) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) isainiwe na daktari wa Wilaya
- iii) Hati ya utii na sheria

Tafadhali soma kwa makini maelezo au magizo haya na kuyatekeleza kikamilifu .

KARIBU SANA KIFARU SEKONDARI

Saini ya Mkuu wa Shule

Jina la Mkuu wa Shule

Mhuri wa Mkuu wa Shule.....

**FOMU YA UTAMBULISHO.
MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI**

SEHEMU A :- Ijazwe na Mwanafunzi

Jina la Mwanafunzi (Majina matatu)

.....

Anwani :.....

Taifa / Uraia

Dini :

Tarehe ya kuzaliwa :Jinsia

Shule anakotoka (Shule ya Msingi) :.....Kata ya

Mwaka wa kumaliza darasa la saba :.....

Wilaya anakotoka :

Mkoa :

SEHEMU B (Ijazwe na Mzazi / Mlezi)

Jina la Mzazi / Mlezi (majina Matatu)

.....

Anwani ya Mzazi / Mlezi:.....

Namba ya simu ya Mzazi /Mlezi :.....

Mahali anapoishi :.....

Kazi ya Mzazi /Mlezi :.....

Mahali anapofanyia kazi :.....

Ndugu wawili wa karibu (wanaoweza kushika nafasi ya Mzazi / Mlezi)

i).....Simu.....

(ii)..... Simu.....

FOMU YA KUKIRI /UTII NA SHERIA.

SHULE YA SEKONDARI KIFARU
S.L.P. 163
MWANGA

TAREHE:.....

MimiMzazi / Mlezi wa
Nimesoma kwa makini Sheria kama zilivyoandikwa katika Maagizo kwa wazazi na nazikubali Sheria hizo na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazingatia kwa manufaa ya Umma.

Mimi(majina ya mwanafunzi)
Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii na kujua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

.....

.....

Saini ya Mwanafunzi

Saini ya Mzazi /Mlezi

Tarehe :.....

Tarehe :

N.B. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza.

Karibu Sana Katika Shule hii.

.....
ABDALLAH .S. MOMBOKA
MKUU WA SHULE

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
KIFARU SEKONDARI

A. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi naikubali / siikubali nafasi hii ya kujiunga na shule Sekondari Kifaru . Naahidi kuzifuata na kuzitii sheria na taratibu zote za shule kama zilivyowekwa na uongozi wa shule hii . Na kama nisipozitii nichukuliwe hatua stahiki .

SAINI YA MWANAFUNZI **TAREHE**

B. AHADI YA MZAZI

Mimimzazi wanaahidi kuwa nitamgharamia chakula kwa wakati . Na kama nikishindwa kufanya hivyo nichukuliwe hatua stahiki . Pia naahidi kushirikiana na uongozi wa shule na walimu katika malezi ya mtoto wangu .

SAINI YA MZAZI **TAREHE**

C. UTHIBITISHO WA MTENDAJI KATA

Mimi Mtendaji wa Kata ya nakubali kuwa namtambua ndugu(mzazi wa mwanafunzi) kuwa ni mkazi halali wa eneo langu la uongozi .

SAINI NA MUHURI WA MTENDAJI KATA TAREHE

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING.

**KIFARU SECONDARY SCHOOL.
P. O. BOX 163,
MWANGA.**

DATE:.....

REF: NO. KHS/MEX/VOL.I/2020

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER,

.....
.....
.....

Please examine (Name of students) who has been selected to join this school for his fitness as a student in the following (To be completed by a medical officer)

- 1. Eye sight**
- 2. Hearing.....**
- 3. Limbs.....**
- 4. SPECIMEN**
 - i) Stool**
 - ii) Urine**
 - iii) Blood**
 - iv) Neurosis**
- 5. Asthma.....**
- 6. Tuberculosis**

- 7. Pregnancy
- 8. Other serious disease:-
 - i) Venereal disease.....
 - ii) Leprosy
 - iii) Epilepsy

MEDICAL CERTIFICATE:

(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above and consider him/ her to be physically fit / unfit as a student .

Date: Signature:

Station : Designation:.....

NB: I request this form to be returned to the school in a sealed – envelop.

.....
THE HEADMASTER